**EPISODE 5 "RECYCLING AND CONSERVING THE ENVIRONMENT"**

---

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu's restaurant. |
| **CUSTOMER** | In his 20's |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George's uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **OMWA** | 19 years old and jobless |
| **MUMBI** | 22 years old, Zapcom's cousin and social worker. |

**<u>INTRO</u>**

1. **<u>MUSIC: THEME MUSIC</u>**

2. **ANNOUNCER** **HUJAMBO MSIKILIZAJI NA KARIBU KWA MAKALA NYINGINE KATIKA MCHEZO HUU WA REDIO** 'LEARNING BY EAR' NOA BONGO

JENGA MAISHA YAKO, HIKI NI KIPINDI CHA 5 CHA MFULULIZO WA HADITHI KUHUSU TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MWASILIANO KWA JINA " UKARABATI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA" '***RECYCLING AND CONSERVING THE ENVIRONMENT'***.

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA ZAPCOM ANAKUMBWA NA WAKATI MGUMU BAADA YA KUFAHAMU KWAMBA ANAHITAJI VIANZO ZAIDI VYA STIMA KATIKA KIBANDA CHAKE ILI KUWAHUDUMIA VYEMA WATEJA.JE TATIZO HILI LITAMFANYA ZAPCOM AKATE TAMAA KATIKA JUHUDI ZAKE ZA KULETA MBADILIKO YA KITEKNOLOJIA MPYA KIJIJINI MWAKE?. ENDELEA KUWA NASI HADI MWISHO WA KIPINDI.

**3. A-SFX: HARD OBJECT MAKES LOUD CONTACT WITH A METAL CONTAINER-A BUCKET**

**SCENE 1: KULA TU FOODS**

**4. UNCLE KILU** Aiiiii kuwa muangalifu …! Umetupa nini katika pipa lile la taka .? Huu ni mgahawa wa Kula tu Foods na wala sio jaa.

5. **ZAPCOM** **(DISMISSING)** Nimetupa simu yangu iliyoharibika. Imekufa kabisa na haifanyi kazi tena. Nimeitumia mpaka imechaka! .

6. **UNCLE KILU** Kwa nini usimpe mtu mwengine, ambaye hawezi kumudu gharama ya simu mpya?. Huwezi kuitupa tu namna hiyo.!

7. **ZAPCOM** Sawa naweza kuwapa watu wengine kama itawasaidia. Lakini sina hakika iwapo kweli itawasaidia. Imekufa kabisa.!

8. **UNCLE KILU** Kwani unamjua mtu … anayeweza kuinunua au kuitumia kama vipuri?

9. **ZAPCOM** (**LAUGHS**) Mzee wewe akili yako iko kwa biashara tu!.Hili si gari kuu kuu ambalo unaweza kulibomoa na kuliuza kama vipuri.

10. **UNCLE KILU** **(NOT CONVINCED)** Nani anayesema hivyo? (**PAUSE**). Bado siamini kwamba kifaa kama hiki cha ghali na kilichochukua muda mrefu kutengenezwa kinaweza kutupwa hivyo tu..kama…kama ganda la ndizi. Unaweza kuitupa katika pipa hili la taka. **(PENSIVE).** Sidhani inafaa tena!

**11. ZAPCOM** (**PENSIVE**) Sawa, naelewa unachomaanisha…na ….na ….

**12. UNCLE KILU** (**JEERING**) Ha…ha…Hatimaye nimekupiku, na kwa mara ya kwanza kabisa umeshindwa kunipa jibu muafaka..Sasa sikiliza kijana, ni wakati wa kunywa supu ya mbuzi…. Nitakuletea supu na wewe endelea na kazi yako ya Komputa tuanze kuuliza maswali. (**SFX FOOT STEPS)** Uliniambia kwamba habari zote za ulimwengu zinapatikana hapa …. katika mtandao huu… nenda .. basi nenda haraka

**13. ZAPCOM** (**MOCKING HIM**) Ndio bosi naenda kwa Komputa bosi!

**14. SFX FOOT STEPS COMING BACK**

**15a. UNCLE KILU** Vyema, ….. sasa unaweza kunywa supu ya mbuzi, huku ukiendelea kututafutia habari kuhusu malighafi inayotumika kutengeneza simu za mkononi na njia salama ya kuitupa inapochakaa au kuharibika **(TO ZAPCOM**) Andika…! sijui ni kuandika au ni kufanya nini..? Na wewe George nisomee nikisikiliza . **(CHUCKLE**) Tumegawana majukumu …sivyo!

**15b. ZAPCOM** Sasa nitaanzia wapi? Niandike nini?, ***....recycle phones (yaani utengenezaji wa simu upya kwa matumizi ya tena na tena,...)***

**15. C-SFX: RAPID TYPING ON KEY BOARD**

**16. GEORGE** Ooh, kuna zaidi ya tovuti milioni moja tunazoweza kufanya utafiti. Ni nyingi sana!.

**17. UNCLE KILU** Fanyeni upesi vijana, sina muda wa kupoteza siku nzima hapa!... na kisha supu ya mbuzi iko tayari jikoni isije ikaungua!.

**18. GEORGE** Subiri kidogo Zap, tunapasa kukagua tovuti hii kwa makini sana!

**19. ZAPCOM** Endelea bado nakusikiliza !

**20. GEORGE** Inaonekana sisi sote tuna simu zinazofanana. Kwa nini tusitafute tovuti ya kampuni inayotengeza simu hizi?.

**21. D-SFX: RAPID TYPING ON KEY BOARD**

**22. ZAPCOM** Sawa habari zote tunaweza kuzipata hapa! **(SILENCE AS THEY READ)**

**23. UNCLE KILU** **(REPRIMANDING)** George, hili ni jukumu lako…. au umesahau ?

**24. GEORGE** **(APOLOGETIC)** Samahani mjomba… hebu nikusomee. (**PAUSE AS HE MOVES FORWARD**)

"… Labda unajiuliza, simu zote za mkononi huishia wapi baada ya kutumiwa? au hufanywa nini zinapochakaa? Kwa wakati huu simu nyingi zinazoharibika au kuchakaa baada ya kutumiwa huishia tu ndani ya makabati. Kwa upande mwengine simu hizi hutolewa kwa watu wengine au kubadilishwa na nyingine mpya. Kimsingi, teknolojia ya kuzitengeneza upya simu hizi za mkononi ni jambo geni na nadra sana katika sehemu nyingi ulimweguni. Na hilo ndilo suala tunalolishughulikia kwa wakati huu ili kubadilisha hali hiyo".

**25a. UNCLE KILU** (**IMPATIENT**) … Lakini tovuti hii hainielezi ni vipi ninavyoweza kutupa simu hii ya Zapu iliyochakaa..

**25b. ZAPCOM** Subiri kidogo, kuna tovuti nyinginr hapa …..

**25. E-SFX: RAPID TYPING ON KEY BOARD**

**26a. GEORGE** … simu zilizochakaa bado zina manufaa makubwa. Ingawa simu hizi zisizoweza kutumika tena huoenekana kama taka, manufaa yake bado ni makubwa. Kwani zinaweza kutumiwa tena kama vipuri au malighafi. Dhamira yetu ni kuhifadhi mazingira bora na salama kwa hiyo tunachofanya ni kuwahimiza wenye simu zisizotumika kuzirudisha kwa watengenezaji. Vituo vilivyotengwa kukusanya mikebe hii ya simu ni kama vile, ***flagship stores, municipal collections, industry association's collections***, au ***retailers' campaigns***."

**26. UNCLE KILU** (**MORE IMPATIENT**) Lakini bado sijui nifanye nini na mkebe huu wangu Zapu. Nasikia harufu ya  supu ya mbuzi ikiungua jikoni

**27. ZAPCOM** ….Zaidi……

**28. F-SFX: RAPID TYPING ON KEY BOARD**

**29. GEORGE** Hebu subiri … kuna mchoro hapa unaoonyesha vifaa mbalimbali vya simu zilizotengenezwa upya na matumizi yake..

**30. UNCLE KILU** (A LITTLE RELIEVED) … Sasa tumeanza kufanikiwa .. Unangoja nini…endelea kusoma soma!

**31. GEORGE** …Betri ya simu hutengenezwa kutokna na madini aina ya Koltan, Nikeli , Shaba na malighafi nyinginezo . Vyote hivi vinaweza kutumika tena kutengeneza Betri, vyuma na vyombo vya kupaza sauti na kadhalika..

**32. UNCLE KILU** Sasa … hivi vyote vinatusaidia vipi….. Ahhh ….supu yangu inakauka!

**33. GEORGE** Ukosi wa dhahabu na shaba (CHUCKLES) unaweza kutumika tena kutengeneza mapambo ya vito, bidhaa nyingine za elektoniki, medali na kadhalika. .

**34. UNCLE KILU** (**LOSING IT NOW**)…Lakini bado sielewi ni vipi itamsaidia mtu wa mashambani kama mimi, kudumisha usafi wa mazingira anapotaka kutupa mkebe wake wa simu…kwa mfano katika pipa hili la taka hapa mgahawani.!!

**35. ZAPCOM** Subiri mjomba, nahakika tukipata ukweli wa mambo, bila shaka hatutakosa njia…maana penye nia pana njia.. endelea kusoma George!

**36. GEORGE** Vibandiko vya plastiki kwenye simu hizi za mkononi… vinaweza kutengenezwa na kutumika tena kama misonobari barabarani, bampa za magari na kujenga au kwa kutumia vizingiti vya plastiki.

**37. UNCLE KILU** Sasa unaona…! haya yote yaliyoandikwa hapa ni kwa manufaa ya watu wa mataifa ya magharibi…sio barani Afrika!. Zapcom hebu nenda ukatupe mkebe wako wa simu huko nje… Hatuwezi kupata usaidizi wowote hapa!. Supu yangu lazima imekauka sasa!

**38. G-SFX HEAVY FEET SHUFFLE AS HE WALKS AWAY MUTTERING.**

**39. UNCLE KILU** **(MUTTERING)** Bampa za magari? Sasa ni nani mwenye gari hapa!

**40. GEORGE** Tufanyeje sasa?

**41. ANNOUNCER** Imebainika kwamba shinikizo la kuweka mazingira safi na salama kwa kutupa simu za mkononi za zamani kwa njia iliyo salama miongoni mwao lipo!. Sasa wamepata elimu. Lakini elimu hiyo bado haijaanza kuwasaidia. Zapcom na George wanatumia fursa hii kushauriana zaidi na marafiki wengine.

**SCENE 2 AT MUMBI'S SMALL OFFICE. SFX: OFFICE SOUNDS**

| | | |
|---|---|---|
| **42.** | **MUMBI** | Asanteni sana kwa kufika hapa ofisini kwangu. Nafikiri kongamano hili linatupa fursa nzuri ya kutafakari na kutafuta njia bora na salama za kutupa simu zisizotumika tena au tuseme ……mikebe ya simu!. Nasikia kwamba malighafi inayotumiwa kutengenezea simu inaweza kuwa sumu? |
| **43.** | **GEORGE** | Lakini yangu ni simu moja tu. Nadhani sumu inayotoka kwa simu moja haiwezi kudhuru ulimwengu mzima! |
| **44.** | **MUMBI** | (**IRRITATED**) Usiseme hivyo George! Chukulia kwa mfano Marekani pekee, unajua kwamba maelfu ya simu hutupwa kila siku! |
| **45.** | **GEORGE** | Lakini huko ni Marekani |
| **46.** | **ZAPCOM** | Pia barani Afrika idadi ya watu wanaotumia simu za mkononi inazidi kuongezeka. Watu wengi sasa wamekumbatia teknolojia hii mpya na kampuni nyingi kutoka mataifa ya magharibi sasa yanatengeneza bidhaa na kutoa huduma ambazo tunaweza kuzimudu, kwa sababu wanajua soko kubwa liko hapa barani Afrika.. |

**47. MUMBI** (**IMPRESSED**) Wow, Professa Zapcom!.Ulipata wapi habari hizi? Usiseme kutoka kwa shangazi yako Bongi..... ...

**48. ZAPCOM** Kuna taka nyingi za elektroniki zinazochafua mazingira. Kumbuka pia sisi hapa barani Afrika huletewa komputa kuu kuu kutoka mataifa yaliyostawi na kuunganishwa tena hapa, na mwishowe sisi ndio tunaoathirika zaidi na sumu inayotokana na taka hizi.

**49. GEORGE** (**SAD**)Kwa sababu hiyo, hatuwezi kutupa mkebe wako wa simu vivi hivi tu hapo nje

**50. MUMBI** Zaidi ya hayo, kadri idadi ya watu wanaotumia simu za mkononi inavyozidi kuongezeka barani Afrika, ndio hatari ya kiwango cha sumu inavyozidi kuongezeka.

**51. ZAPCOM** Kuna zaidi ya hayo....

**52. GEORGE** Ohhhhh , tatizo letu kwa sasa hivi ni kupata njia bora na salama ya kutupa mkebe huu mmoja tu wa simu, na wala sio kuokoa ulimwengu mzima!.

**53. MUMBI** Ama kwa hakika mnatimiza jukumu lenu katika kuuokoa ulimwengu. Mnajua kwamba utandu wa Mbale aina ya chuma unaotumiwa kutengeneza simu za mkononi na bidhaa nyingine za Elektroniki hutokana na madini aina ya Coltan.

**54. ZAPCOM** Coltan?

**55. MUMBI** Ndio neno muafaka kwa madini aina ya ***Columbite Tantalite***. Na madini haya hupatikana kwa wingi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Ni jambo la kusikitisha kwamba watu walafi na wenye ubinafsi huchimba madini haya na kuyauza kwa lengo la kununua silaha ili kuendeleza vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo.

**56. GEORGE** Ooh ni jambo la kuhuzunisha sana! Sisi tulitaka tu kupata njia salama ya kutupa mkebe huu wa simu na sasa tumeingilia masuala ya mizozo ya kivita ulimwenguni. Kwani tumekuwa Umoja wa mataifa? (MEEKLY). Hii ni simu tu.

**57. MUMBI** Kwa hakika katika mazingira ya vita mambo mengi hutokea. Misitu kunakopatikana madini haya pia imeharibiwa na hakuna juhudi zozote za kupanda tena miti.

**58. GEORGE** Sasa tumekuwa Wangari Mathai, yule mwanamazingira mashuhuri nchini Kenya ambaye alipata tuzo la amani la Nobel. Sijui ni kwa nini tunazungumzia mambo haya yote, tatizo letu kubwa hapa ni kupata tu njia bora na salama ya kutupa simu hii ndogo na isiyofaa!

**59. ZAPCOM** (**VERY PENSIVE**) Tunaweza kulichukulia suala kuwa dogo na linalopasa tu kujadiliwa na watu wa vijijini kama sisi barani Afrika, lakini maisha ya siku za usoni yako mikononi mwetu sote sisi vijana.

**60. (SILENCE)**

**61. GEORGE** Kwa hivyo tufanye nini sasa ?

**62. ZAPCOM** Mbali na kuagiza supu ya mbuzi uipendayo, napendekeza tutazame tovuti zote za kampuni zinazotengeneza simu za mkononi na tuwaulize jinsi wanavyoweza kutusaidia. Kampuni nyingi zina wawakilishi wao katika miji mikubwa kote hapa barani Afrika. Huwezi kujua, labda kampuni hizi zinaweza kutupatia kandarasi ya kukusanya simu kuu kuu na kuwapelekea. Lakini kwa wakati huu nitaihifadhi simu hii ya zamani hadi tutakapopata njia bora na salama ya kuishughulikia.

**63. MUMBI** Hilo ni wazo zuri sana, hebu sasa twendeni!

**64. H-SFX: TAPPING OF KEY BOARD**

**65. ZAPCOM** George, una mpango gani sasa ?

**66. GEORGE** Kuagiza supu ya mbuzi kwa kupitia ujumbe mfupi yaani sms!

**MUSIC: THEME MUSIC**

**67. OUTRO**

**68. ANNOUNCER** Kile kilichoonekana kuwa suala dogo tu kwa kudni hili la Vijana katika kutafuta njia bora

na Salama ya kutupa mikebe ya simu, sasa limegeuka kuwa suala la usalama wa mazingira kote ulimwenguni.Na zaidi wanaridhika na wajibu wanalotekeleza. Wamejifunza kwamba licha ya umri wao mdogo na kijiji wanakotoka, wanajukumu kubwa la kutekeleza katika kuhifadhi mazingira ulimwenguni. Teknolojia mpya ya habari na mawasiliano imewafungua macho, lakini pia wanafahamu jukumu kubwa wanalopasa kutekeleza. Ni kupitia teknolojia hii ya mawasiliano ambapo wameweza kupata habari muhimu na jinsi wanavyoweza kuwashawishi vijana wenzao kuwa na mwelekeo bora. Lakini je watafaulu katika jitihada zao?.

**ANNOUNCER** Basi kufikia hapo ndipo tunapofika mwisho wa kipindi cha Leo. Ungana nasi kwa makala nyingine ijayo ili upate kufahamu kile kitakachotokea. kwa maelezo zaidi kuhusu kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Na iwapo una maoni usisite kututumia nasi itakuwa furaha yetu kuyapokea. Hadi wakati mwengine tutakapoungana na makala nyingine Kwaheri kwa Sasa.